# *WASHA TAA*

Vema. Je! hii ndiyo . . . [Ndugu fulani anasema, "*Hii* ndiyo maikrofoni yako."—Mh.] Hii ndiyo kubwa? Asante, bwana. ["*Hii* ndiyo maikrofoni inayofanya kazi."] Naam, bwana. Vema. Ninaona walikuwa wakipata mwangwi kidogo pale nyuma, na kwa hiyo . . . Habari za asubuhi, wapendwa. Je! mnaweza kunisikia vizuri huko nyuma? [Kusanyiko linasema, "Ndiyo."] Hiyo iliuondoa. Asanteni.

2 Bila shaka mimi ni mtu aliyejaliwa, asubuhi ya leo, kuja hapa kwenye jukwaa hili, baada ya shuhuda nzuri namna hii kutolewa; kujaribu ku—kuweka kidogo tu zaidi pamoja na yale wamesema, kutuletea baraka kama tulizofurahia asubuhi ya leo. Sasa, naliona baadhi yao walikuwa ninii sana . . .

3 [Mfumo wa upazaji sauti unarudisha mwangwi wa sauti. Ndugu fulani anasema, "Nafikiri itatubidi kuiweka, hii, katikati, Ndugu Branham."—Mh.] Vema, bwana. Je! hivyo ni bora zaidi?

4 Tukiwa na baadhi ya hawa watu hapa, jinsi wamezungumza, na karibu kila mmoja . . . Vema, kila mmoja hapa juu alikuwa na ushuhuda mzuri sana, wa kuchangamsha. Jinsi ninavyofurahia jambo hilo, huo ushuhuda mzuri kwa ajili ya Bwana!

Sasa tutaliendea Neno.

5 Nami, juma hili, nimekusudia moyoni mwangu kutowaweka watu saa hizi mbili ama tatu, wameketi, wakinisikiliza. Nitawaambia ni kwa nini ni—ninafanya hivyo, enyi ndugu. Mimi sina elimu, na ninaweza tu kuzungumza kwa uvuvio. Sasa, mtu mwenye elimu, wakati anapovuviwa, pia; bali anaweza kuelezea yale anayozungumzia habari zake, kwa elimu yake, kutoa maneno ambayo yatawafanya watu wajue yale anayozungumzia. Bila elimu, inanibidi kuchukua mifano ya maumbile na kuielezea kwa uvuvio nilio nao. Na hilo linafanya mambo kuwa magumu sana, mara nyingine, kwa watu kweli kuelewa. Tunaona ya kwamba lilinisumbua sana mpaka nikakuta kwenye Biblia ya kwamba Mungu alifanya vivyo hivyo, njia zizo hizo.

6 Tunaona, kama vile Yohana Mbatizaji, wakati hatuna taarifa yo yote ya elimu yake, na halafu, wakati yeye—wakati alipotoka nyikani, alianza kulizungumzia ku—ku . . . kusanyiko lake, kanisa la siku zile. Nasi tunaona jinsi alivyolielezea. Alisema, "Enyi wazao wa nyoka." Unaona, hao ndio aliowazoea, maumbile na nyika; kwa maneno mengine, kitu ambacho ni kijanja na cha kuteleza, na kidanganyifu. Sasa, watu wengine huenda wangaliweza kuleta neno fulani ambalo lingalisema "walaghai" ama neno fulani ambalo angaliweza kutumia

kuelezea hilo. Lakini Yohana alitumia neno "nyoka." Nafikiri kila mtu alielewa aliyoyazungumzia.

7 Kwa hiyo basi alisema, "Msianze kufikiri kusema nafsini mwenu, ya kwamba, 'sisi ni wafuasi wa *hili* na ni wafuasi wa *lile*,' maana nawaambia, Mungu anaweza kutoka katika mawe haya hapa," unaona, unaona, si vitu fulani vingine vikubwa fulani. "Mungu anaweza kutoka katika mawe haya." Yeye alilielezea hilo katika maumbile.

8 Na, pia, "Shoka limewekwa kwenye shina la mti." Ndugu fulani mzuri mwenye elimu, akiwa na uvuvio uo huo, huenda angalisema, "Ataangamiza." Yeye alisema, "Shoka liko kwenye shina la mti." Huko ni kuuangamiza, hata hivyo, unaona, kwa hiyo yeye—yeye alijua kwamba ilikuwa hivyo. Alikuwa tu na usemi huo, kwa kuwa labda hakuwa na kisomo cho chote.

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu.

9 Nina haja hapa za maombi. Ambapo, hiyo ndiyo huduma yangu, kuwaombea wagonjwa. Nina haja chache zilizoletwa hapa, maombi muhimu sana. Nami ninajua kuna wengi hapa. Na endapo wapo wengine, asubuhi ya leo, ambao wangetaka kukumbukwa? Vema, kama utamwinulia tu Mungu mikono yenu, useme, "Mimi. . . " Sasa shikilia tu ombi lako tunapoomba.

10 Baba yetu wa Mbinguni, sasa tunaukaribia Utakatifu Wako, kwa Jina la Mwanao Mtakatifu, Bwana Yesu, kuomba ombi hili, la kila mmoja wa watu walioandika maombi yao, niliyo nayo hapa mkononi mwangu. Hasa sana binti mzuri wa maskini ndugu huyu ambaye amechanwa katika ile ajali. Ninamwombea mtoto huyo, Bwana. Na ninaombea haja nyingine zote. Na yale ambayo ni ya siri sasa kwetu, kwa wale tu walioinua mkono wao; bali Wewe ni Mungu asiye na kikomo, na unajua kila kusudi na maombi yetu yote. Tunaomba ya kwamba utajibu. Kwa sababu umeahidi jambo hilo, tunaliamini.

11 Na tunaomba sasa ya kwamba Wewe utayachukua maneno haya machache ambayo tutasoma, na utuvuvie nayo, Bwana, tunapokungoja Wewe. Jalia Roho Mtakatifu amkaribie kila mmoja, na kutufunulia fasiri ya Neno. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

12 [Kuhusu maikrofoni, ndugu fulani anasema, "Ndugu Branham, je! tungeweza kufanya jaribio tuone kama itafanya kazi?"—Mh.] Naam, bwana, ndugu, endelea tu. Hilo ni sawa. Ninapofungua sasa, nina ninii . . .

13 Zamani ilikuwa kwamba niliweza kuyakumbuka Maandiko yangu na mambo mengine mengine, bila ya kuwa na—na muhtasari, lakini tangu nilipopitisha miaka ishirini na mitano, hilo halifanyi kazi vizuri sana. Inanibidi kuyakumbuka kwa kuyaandika. Sasa tunaenda . . .

14 Hivyo ni bora zaidi? Mnaweza kunisikia vizuri zaidi? La. Huko nyuma, wanatikisa vichwa vyao. Labda… [Ndugu fulani anasema, "Inakubidi kusimama moja kwa moja mbele yake."—Mh.] Inanibidi kusimama… ["Moja kwa moja mbele yake."] Sawa. Na ingekuwaje namna *hii*, je! mnaweza kusikia ikiwa hivyo? Na *hivyo* je! hilo ni afadhali? Sawa. Hivyo ni sawa.

15 Sasa ningetaka kuwaelekeza kwa—kwa Isaya 42:1-7, na pia kwa Mathayo 4:15-16.

> *Tazama mtumishi wangu nimtegemezaye; mteule wangu, ambaye nafsi yangu imependezwa naye; nimetia roho yangu juu yake; naye atawatolea Mataifa hukumu.*
>
> *Hatalia, wala hatapaza sauti yake, wala kuifanya isikiwe katika njia kuu.*
>
> *Mwanzi uliopondeka hatauvunja,…utambi utokao moshi hatauzima; atatokeza hukumu kwa kweli.*
>
> *Hatazimia, wala hatakata tamaa, hata atakapoweka hukumu duniani; na visiwa vitaingojea sheria yake.*
>
> *Mungu BWANA anena, yeye aliyeziumba mbingu, na kuzitanda; yeye aliyeitandaza nchi na mazao yake; yeye awapaye mkate watu walio juu yake; yeye awapaye roho wao waendao ndani yake.*
>
> *Mimi, BWANA, nimekuita katika haki, nami nitakushika mkono,…kukulinda, na kukutoa uwe agano la watu, na nuru ya mataifa;*
>
> *Kuyafunua macho ya vipofu, kuwatoa gerezani waliofungwa, kuwatoa wale walioketi* magerezani *katika nyumba ya kufungwa..*

16 Na sasa katika Mathayo Mtakatifu 4, kuanzia na kifungu cha 12, tunasoma haya.

> *Basi Yesu aliposikia ya kwamba Yohana amefungwa, alikwenda zake mpaka Galilaya;*
>
> *Akatoka Nazareti, akaja akakaa Kapernaumu, mji ulioko pwani, mipakani mwa Zabuloni na Naftali:*
>
> *Ili litimie neno lililonenwa na nabii Isaya, akisema,*
>
> *Nchi ya Zabuloni na nchi ya Naftali, njia ya bahari, ng'ambo ya Yordani, Galilaya ya Mataifa,*
>
> *Watu wale waliokaa katika giza wameona mwanga mkuu, nao waliokaa katika* nchi za uvuli *wa mauti mwanga umewazukia.*
>
> *Tokea wakati huo Yesu alianza kuhubiri,…kusema, Tubuni; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia.*

17 Bwana na abariki Neno Lake! Sasa somo langu asubuhi ya leo ni: *Washa Taa*. Na upesi tu niwezavyo, ili mweze kutoka kwa

ajili ya mkutano huu mwingine sasa, ambao utafanyika katika muda wa dakika arobaini na tano hivi.

18 Mnajua, Bw. Mc Anally, nafikiri yupo. Niliona lori lake kubwa nje. Wakati fulani uliopita, tulikuwa tumeketi, moja ya ziara zangu za kwanza hapa ya kwenda Arizona, kwenda kuwinda. Tulikuwa tumeketi hapa nje karibu na mlima wa ushirikina. Nilikuwa nimesikia habari zake kwa muda mrefu sana, na kusikia hekaya nyingi zilizokuwa zimesimuliwa kuhusu huo wa Ushirikina. Ninakumbuka nilikuwa nikiutafuta, mara ya kwanza; ilikuwa ni kabla ya mapambazuko, na kivuli kikubwa cha kizuka kilining'inia upande wangu wa mashariki, ambacho kilijulikana kama Ushirikina. Nilikuwa nimesikia juu ya Wahindi, jinsi ambavyo wasingeweza kuukaribia, jinsi ambavyo walihofu, jinsi ambavyo Wahispaniola walivyokuwa wamewatenda mabaya katika siku za mwanzoni walipokuwa wakitafuta dhahabu. Walidai ya kwamba pepo wachafu waliishi humo. Haya yote yalichochea udadisi wangu. Lakini nilikuwa na tochi tu, kwa ajili ya kuuona huo Ushirikina, kwanza.

19 Na ndipo nikaangalia mpaka, baada ya kitambo kidogo, utukufu wa jua ukaanza kusogea juu ya giza hilo. Na ulipofanya hivyo, ulitenganisha giza na nuru, na kulisukuma giza nyuma. Hatimaye, likapanda katika utukufu wake, juu ya kilele cha huo mlima, na likaonyesha jinsi Ushirikina hasa ulivyokuwa. Liliangaza na kuonyesha ulivyokuwa. Na mizuka yote na hofu niliyokuwa nayo kutokana na Ushirikina, wakati jua lilipokuwa likiangaza kwa nguvu zake juu yake, vyote vilitoweka.

20 Jua ni mfalme wa nuru zote juu ya dunia hii, kuhusu nuru za maumbile. Haidhuru tunaweza kuwa na nuru za kujitengenezea jinsi gani, na ni miali mingapi ya umeme tunayoweza kutengeneza; jua hilo linapopanda, zote nyinginezo zinafifia.

21 Hivyo ndivyo ilivyo kwa Neno la Mungu. Wakati Neno la Mungu linapotokeza, ushirikina wote, ushupavu wa dini wa kimadhehebu na kadhalika, vinatawanyika, na inaonyesha vile hasa hali halisi ya mambo ilivyo. Mungu, hapo mwanzo, alisema, "Iwe nuru." Nuru huja tu, Nuru halisi, Nuru kuu, huja kwa Neno la Mungu. Mungu alitenganisha nuru na giza, hapo mwanzo. Nalo Neno la Mungu, lililodhihirishwa, daima hutenganisha Nuru na giza.

22 Watu wanaweza kuinuka wakiwa na *hiki*, *kile*, ama na *kingine*; itikadi zinaweza kuzuka, ukomunisti, ufashisti, na itikadi zingine zote zinaweza kuzuka; ushirikina, vikundi, cho chote kile, huenda kikazuka. Lakini wakati hiyo Nuru kuu ya Biblia inapozuka, ushirikina wote na kadhalika... Lakini, unaona, tunajua hiyo iko, bali mpaka itakapothibitishwa, tutahakikisha Nuru Yake; basi hatuna haki ya kubishana dhidi ya jambo hilo, kwa maana inafungia nuru zingine zote nje. Yesu

alisema, "Kila neno la mwanadamu na liwe ni uongo, na Langu liwe Kweli." Neno Lake ni kuu juu ya maneno mengine yote ya mwanadamu, juu ya yote, cho chote kile. Neno Lake ni Nuru.

23 Nasi tunajua kwamba hapo mwanzo hapana budi kulikuwa ni ukungu na huzuni na giza, dunia ilipokuwa ikizunguka, na ndipo Mungu alipojua ya kwamba alikuwa na haja ya nuru. Sasa, mbegu Yake ilikuwa tayari iko ardhini, kwa maana Yeye alikuwa ameipanda hapo. Sasa Yeye alihitaji nuru kuotesha hiyo mbegu, kuifanya hiyo mbegu iishi, kwa maana hiyo mbegu ilikuwa ipo hapo tayari.

24 Ni kama tu vile ilivyo katika kila wakati, Mungu ametutabiria yale yatakayotukia katika kila wakati. Kitu pekee anachohitaji ni kudhihirishwa kwa Nuru ya Mungu juu ya hayo Maandiko, kuyafanya yawe hai kwa ajili ya wakati huo. Ninii tu . . . ? . . . Na hayo yatafanya hivyo almuradi tu Nuru hiyo inaweza kulifikia Neno. Kama Neno limehuishwa, litayafanya kuwa hai kama ni ahadi ya siku hiyo.

25 Unaweza ukapanda ngano wakati mmoja, ama nafaka katika wakati mwingine. Zingine humea pole pole kuliko zingine, kwa sababu inategemea msimu.

26 Neno la Mungu huja katika msimu wake, torati na neema, na kadhalika, kama tulivyopitia kwenye nyakati mbalimbali. Na, kila wakati, unamulikwa na dhihirisho la Nuru ikisambaza U— Uhai ulio katika hiyo Mbegu.

27 Kwa Neno la Mungu, jua linawaka leo, kwa sababu jua lili hili tunalolifurahia ni Neno la Mungu lililodhihirishwa. Nuru hii yenyewe ya jua tunayoona hapa nje si kitu ila ni Neno la Mungu, wakati Yeye aliposema, "Iwe nuru."

28 Na vipi kama Yeye alikuwa amesema, "Iwe nuru," wala hapakuwapo na nuru? Basi si Mungu aliyekuwa amenena. Mungu anaposema, "Iwe," itakuwa. Na kwa hiyo tunaona ya kwamba jua ambalo tunafurahia sasa ni dhihirisho la Neno la Mungu lililonenwa katika Mwanzo.

29 Nasi tunatambua ya kwamba Nuru ya Mungu ya siku ya leo ni Mwanawe. Moja ya hizo ilikuwa ni j-u-a; huyu ni M-w-a-n-a. M-w-a-n-a ni Biblia. Yeye alikuwa . . . "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu." Waebrania 13:8, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Ni Neno la Mungu, daima. Ilikuwa ni Kristo katika Nuhu. Ilikuwa ni Kristo katika Musa. Ilikuwa ni Kristo katika Daudi aliyeangalia juu, kama mfalme aliyekataliwa, juu ya ule mji; ambapo, miaka mia nane baadaye, Kristo aliketi pale akiulilia mji, akiwa ni Mfalme aliyekataliwa, kama tu vile Daudi alivyokuwa. Daima ni Roho wa Kristo. Na dhihirisho kamili la Neno la Mungu lilifanywa dhahiri kupitia kwa Yesu Kristo, Roho wa Mungu.

30 Hakuna uhai unaoweza kuja nje ya nuru. Nuru huzaa; nuru huzaa uhai. Hakuwezi kuweko na uhai—uhai nje ya nuru, ya kawaida ama ya kiroho. Inapaswa kuwapo.

31 Na Nuru tu ndiyo inayoweza kuja kwa Neno la Mungu. Neno la Mungu ndiyo Nuru wakati limedhihirishwa. Ni Mbegu tu inayokaa pale, kama vile Mungu alivyopanda mbegu zote.

32 Miili yetu ilikuwa duniani kabla ya ninii . . . vema, vema, kabla hapajakuwapo na nuru yo yote hapa, uhai wo wote hapa, au cho chote kile; ile kalisi, potashi, petroli, na nuruulimwengu, cho chote, vilikuwapo hapa—vilikuwapo hapa wakati Mungu alipoiumba nchi. Ilihitaji tu Neno Lake lililonenwa kukifanya kiwepo, kama tu vile ilivyofanyika kwa uhai wa mimea, ama uhai wa mti, ninii, ama uhai wo wote unaopaswa kuwapo.

33 Hakuna kitu kinachoweza kuishi, cha kimaumbile ya kawaida ama cha kiroho, bila ya Nuru Yake, nalo Neno Lake ni Nuru na Uzima.

34 Lakini wakati anapoituma Nuru Yake na kuifanya ijulikane kwa watu, na halafu inakataliwa, basi ni vipi kuhusu jambo hilo? Hilo ndilo tunalotaka kuzungumzia asubuhi ya leo, ni: kuikataa Nuru hii, na wale ambao ilitumwa kwao, wanaikataa kama tu ilivyokuwa wakati ule. "Tazama mtumishi Wangu, nimtegemezaye." Yeye ni Nuru kwa Mataifa. Yeye ni nuru kwa ulimwengu. Alikuwa ni Nuru ya ulimwengu, bali alikataliwa. Hiyo ndiyo sehemu inayohuzunisha.

35 Na inakutana na hali hiyo kila wakati ambapo Mungu anadhihirisha Nuru Yake, ulimwengu wenyewe unaikataa nuru hiyo. Kwa nini? Imeandikwa moja kwa moja katika Biblia. Kila wakati, Mungu amegawa kiasi fulani cha Neno Lake kwa ajili ya kila kizazi, Naye daima humtuma mtu mmoja kudhihirisha Neno hilo.

36 Yesu alikuwa ametabiriwa kwa muda wa miaka elfu nne, ya kwamba angekuja, Masihi. Na wakati alipokuja, alidhihirisha kila ahadi ya Masihi. Lakini hata hivyo watu wa dunia, makanisa, na kadhalika, hawakujua kitu cho chote juu Yake, kwa hiyo, maana tayari walikuwa wamekwisha kuingia katika jambo lingine lililowazuia wasijue jambo Hili. Sasa vipi kama—kama mtu ananinii tu . . .

37 Tutachukua upande wa maumbile ya kawaida. Vipi kama mtu, ambaye amezaliwa hapa apate kutembea katika nuru ya hilo jua, kile ambacho Mungu amemwumbia, na, muda si muda unajua, yeye anafumba macho yake, anakimbilia kwenye chumba cha chini ya nyumba, anafunga mlango, anashusha mapazia, na anakataa kabisa kutambua kwamba jua linawaka? Anakataa baraka zake. Anakataa miali yake inayotia joto, nguvu zake za kutoa uhai. Anakataa nuru ambayo linaisambaza apate kuona anakoenda, mahali alikotoka. Anakana hayo. Ungesemaje kuhusu mtu aliyeshusha mapazia, ama aliyekimbilia kwenye

chumba cha chini ya nyumba na akaifungia nuru yote nje, kila mahali, na vivi hivi tu amekataa kutambua ya kuwa jua lilikuwa linawaka? Mtu huyo ana kasoro fulani kiakili. Mtu ye yote anajua hilo. Akili za kawaida zitakwambia kuna kasoro fulani kwa mtu huyo, ya kwamba yeye ni, yeye ni—yeye ni . . . Jambo fulani limetukia kwake. Ana wazimu.

38 Vema, hivyo ndivyo ilivyo katika saa tunazoishi, wakati mtu atajifunika na namna fulani ya—ya udhuru, kutambua kwa kweli Nuru ya Injili inapoangaza kama ilivyo leo. Wakati mtu anapoipuuza makusudi, anaingia katika jambo fulani na kushusha pazia, aseme, "Siamini jambo Hilo," mtu huyo ana kasoro. Hakuna njia kamwe ya kulitatua jambo hilo. Kuna kasoro. Jambo fulani limempata. Nasi tunaona ya kwamba kuna ninii sana, mengi sana ya mambo hayo siku hizi.

39 Sasa, Yesu alikuwa ndiye shuhuda zote zilizovuviwa za manabii. Na unabii wao wote ulifunuliwa katika wakati Wake, ambao ulikuwa umetabiriwa kwa ajili ya wakati Wake. Yeye aliwasha kila taa ya Neno lililokuwa katika Biblia, ambalo lilitabiriwa juu Yake. "Bikira atachukua mimba." Alichukua mimba. Vema. "Ataitwa Jina Lake Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa Milele." Yeye alikuwa hivyo. "Na macho ya vipofu yataona." Yaliona. Kila kitu kilichotabiriwa juu Yake, kilitukia wakati alipokuja duniani.

40 Na sababu ya watu kutoweza kuona jambo hilo, ilikuwa ni kwamba . . . Linaonekana ni la kushangaza kwetu sasa, kwa sababu tunaangalia kupitia kwenye kioo cha kutazamia nyuma. Lakini je! ulipata kujua, ukiendelea kuangalia nyuma hivyo, utapata ajali? Hebu na tuangalie yaliyo mbele zetu.

41 Hivyo ndivyo walivyokuwa wakifanya. Sababu ya wao kufanya hivyo, ni kwa sababu walikuwa wakiishi katika mng'ao wa nuru nyingine. Walikuwa wakiishi katika mng'ao wa nuru ya siku nyingine.

42 Na hiyo ndiyo sababu ninaamini hiyo ndiyo shida uliyo nayo ulimwengu leo, wapendwa, ni kwa sababu tunajitahidi kuishi katika mng'ao wa nuru iliyoangaza katika siku nyingine. Mng'ao ni nuru danganyifu.

43 Ni kama tu mazigazi barabarani. Tunashuka kwenda barabarani na kuona mazigazi. Ni picha ya bandia ya jua. Na unapofika pale, haijadhihirisha kitu ila kitu cha uongo. Kwa sababu, huwezi kutembea katika mmweko wa jua, kwa sababu ni mazigazi, daima yakikuonyesha kitu fulani ambacho ni uongo mtupu.

44 Na wakati watu wanapojaribu kukwambia ya kwamba Yesu Kristo si yeye yule jana, leo, na hata milele, wanakuongoza kukuingiza katika mazigazi. Hivyo tu. Na wakati unapoingia katika kanisa na kujiunga na kanisa, kanuni fulani baridi ama

kitu kama hicho, hakuna kitu hapo, si zaidi ya yale uliyokuwa nayo duniani.

45 Hebu nikwambie. Usiikatae Nuru ya Injili ya Yesu Kristo, ambayo inaleta miali inayotia joto ya Roho Mtakatifu juu yako, inakufanya kiumbe kipya katika Kristo Yesu. Usijaribu kutembea katika mng'ao fulani wa wakati mwingine. Sasa, mng'ao huo huenda ulikuwa ni sawa katika wakati mwingine, huenda ulikuwa ni sawa kwao.

46 Ilithibitika kuwa hivyo katika siku ya Bwana wetu Yesu. Yeye alikuwa ndiye Nuru ya Kimaandiko ya siku hiyo. Alikuwa ndiye ile Nuru. Yeye hakuwa ile Nuru mpaka alipokuja duniani kuthibitisha Neno lililoahidiwa. Unajua, Yeye alisema pale, "Yohana alikuwa ni nuru angavu na inayong'aa, nanyi mlipenda kutembea katika nuru yake kwa muda."

47 Bila shaka, kwa sababu Yohana alikuwa ametabiriwa na Isaya, miaka mia saba na kumi na miwili kabla ya kuzaliwa kwake, ya kwamba, "Sauti ya mtu itakuwa ikilia nyikani." Na pia Malaki, wa mwisho wa wale manabii, miaka mia nne kabla ya kuja kwake, katika mlango wa 3 wa Mal-. . . wa Malaki, yeye alisema, "Tazama, namtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu, kuitengeneza njia."

48 Huyu hapa Yohana duniani, akilifanya Neno hilo lililoandikwa liishi. Alikuwa ni sauti ya mtu aliaye nyikani, na yeye daima. . . pia alikuwa akiitengeneza njia mbele ya Masihi. Na Yesu alisema, "Mlipenda kutembea katika nuru yake, kwa sababu Yeye alikuwa ndiye ile nuru, inayong'aa na kuangaza."

49 Naye Yohana, alisema, "Sasa sina budi kupungua, nuru yangu haina budi kuzima, kwa sababu (kwa nini?) nimemaliza kutumikia wakati wangu uliotabiriwa juu yangu. Msikieni Yeye! Yeye Ndiye wa kumsikia. Mfuateni." Hiyo ikiishi katika siku hiyo, ilithibitisha jambo hili.

50 Sasa, Wayahudi walidhani ya kuwa walikuwa wakiabudu katika nuru ya kweli. Walidhani walikuwa wakimwabudu, Mungu yuyu huyu waliyekuwa wakimkataa. Yeye yule waliyedhani kwamba walikuwa wakimwabudu, walikuwa wakimsulibisha. Walikuwa wakimdhihaki Mungu yeye yule, na kumfanya mtu wa kuchekwa na watu, Mungu yeye yule waliyedhani walikuwa wakimwabudu.

51 Hebu niseme jambo hili kwa uchaji na heshima, si lo lote bali ni kuleta Nuru tu, kwa sababu, kama vile ndugu yetu alivyosema muda mfupi uliopita, tunaishi ambapo tumechelewa sana kuliko mnavyodhania tuna muda. Moja ya siku hizi jambo fulani litatukia, itakuwa tumeisha chelewa. Watu watachukua alama ya mnyama, bila hata kujua yale wanayofanya. "Kipofu akimwongoza kipofu mwenzake, wote wanaanguka shimoni," Yesu alisema. Nasi tunaishi tukiwa tumeisha chelewa kuliko

tunavyofikiria. Watu wengi waaminifu wanafuata hayo, bila hata kujua wanalofanya.

52 Lakini wakati umewadia sasa wakati Nuru inaangaza, Nuru ya Injili, katika nguvu Zake za kufufuka kwa Yesu Kristo, akijidhihirisha ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Yeye alipangia hilo kwa ajili ya siku hii. Mambo aliyoahidi kwa ajili ya siku hii hayana budi kutimia katika siku hii. Kama kanisa halitakubali jambo Hilo, Mungu anaweza kutoka katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto. Ataufikisha Ujumbe Wake, kwa maana daima ameufikisha. Daima atafanya jambo hilo.

53 Watu wakifikiri ya kwamba wanatembea katika Nuru, mapokeo ya baba zao, na, muda si muda unajua, wanatembea katika mweko wa nuru, si Nuru ile ile, wamekataa Nuru ile ile wanayodai kuwa wanaiabudu.

54 Kazi Zake zilimthibitisha kwelikweli kwamba Yeye alikuwa ni Nani. Yesu alisema, Mwenyewe, "Yachunguzeni Maandiko, kwa kuwa mnadhani ndani Yake mna Uzima wa Milele, na Hayo ndiyo yanayonishuhudia. Ni nani anayeweza kunihukumu kwamba nina dhambi?" Alisema, "Ni nani anayeweza kuthibitisha kwamba nimesema jambo lo lote, ama nimefanya dai lo lote, ambalo Baba wa Mbinguni hajathibitisha hilo kwa Mimi?" Amewathibitishia ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Nuru ya saa hii, kwa sababu yote yalikuwa yametabiriwa ya kwamba Masihi huyu anapaswa kuwa hivi, na hapa akachanua katika Uzima, bali mapokeo yao yalikuwa yamewatenganisha na Nuru halisi ya Neno.

55 Mafarisayo, Masadukayo, Maherodia, na cho chote kile, walikuwa wameuchafua ulimwengu sana, kama walivyofanya katika nyakati zote, hata wasingeweza kuona Nuru halisi. Iliwapofusha macho. Walikuwa wamezoea kutembea katika mng'ao, "Kesho yake itakuwa *hivi*, na kesho itakuwa *hivi*. Tutajiunga na *hili*, na itakuwa *vile*. Tutajiunga na *lile*." Tunaona ni mazigazi ya uongo.

56 Yesu Kristo ni halisi tu leo, kwa moyo wa mwanadamu, kama alivyowahi kuwa. Nguvu Zake na Uwepo Wake ulio hai ni halisi tu leo kama ulivyopata kuwa. "Tazama, bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena. Kosmos, 'mfumo wa ulimwengu,' hautaniona Mimi tena. Hata hivyo, ninyi mtaniona; kwa maana nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari. Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya, hata kubwa kuliko hizi mtazifanya, maana ninaenda kwa Baba Yangu."

57 Ahadi hiyo kuu ni leo hii. Watu ni vipofu kupindukia, lakini kuna "ninyi ambao mtaniona," na hilo ndilo tunalojaribu kufikia leo. Kile full Gospel, inachomaanisha, ni kumwonyesha Yesu Kristo katika nguvu za kufufuka Kwake, na utimilifu wote wa

ahadi Zake; ya kwamba Roho Mtakatifu anadhihirisha mambo haya na kuyafanya ni kweli, ambayo Mungu ameahidi, Naye atayatimiza. Naam, bwana.

58 Yeye alikuwa amethibitishwa kwelikweli na Ne—Neno na kazi alizokuwa akifanya, bali hakuna hata mmoja wao aliyetaka kuamini jambo hilo. Alithibitisha Nuru Yake ilikuwa ni Neno! Neno lilisema jambo hilo, "Yachunguzeni Maandiko."

59 Lakini mapokeo yao waliyokuwa wakiishi katika hayo, mweko wa wakati mwingine! Wao walisema, "Tunamwamini Musa; Musa ndiye tunayemwamini. Hatujui unakotoka. Ulipata wapi elimu Yako? Unawezaje kuthibitisha ya kwamba *Hivi* ndivyo ulivyo?"

60 Kazi Zake zilishuhudia kwamba Yeye alikuwa ni Nani, kama tu wangaliisoma Biblia. Walikuwa wakiisoma, bali hawakuweza kuliona jambo Hilo. "Kazi Zangu zinanitambulisha."

61 Mtu anajulikana kwa sifa zake, sifa za Neno la Mungu, kama yeye ametumwa na Neno la Mungu na ana Neno la Mungu. Ndivyo ilivyo katika kila wakati! Imekuwa hivyo daima.

62 Hatuwezi kuishi kwa nuru ya jana. Nuru ya jana ni historia. Hatujui kitu cho chote juu yake. Huwezi kupata joto leo kwa jua linalowaka jana. Hiyo ndiyo shida ya makanisa siku hizi. Hiyo ndiyo shida waliyo nayo watu, wanajaribu kuishi kwa yale yaliyotendeka jana. Huwezi kupata joto kwa moto wa kuchorwa. Hakika huwezi, hauna joto ndani yake. Jua la jana halina joto ndani yake.

63 Nuru ya jua inatumwa duniani, katika maumbile ya kawaida, ipate kuiivisha punje kwa ajili ya mavuno yajayo. Kila siku inaleta jua jipya. Jua linalowaka leo, likiikuza ngano, huko Canada; jua lilo hilo, vema, kama halikuninii. . . haikupigwa na jua zaidi ya hilo, Julai hii ijayo ama Agosti, jua hilo lisingeweza kamwe kuiivisha hiyo nafaka. Halina budi kuwa kali zaidi na lenye nguvu zaidi, kila siku linakua na kukomaa, lipate kuiivisha hiyo nafaka.

64 Sasa kama hiyo punje, yenyewe, kama ikianza kukomaa, punje inajitokeza, kama ikidumu kuendelea kukaa na punje, inaiendeleza tu hiyo punje. Kila siku, hilo kapi linaloifunika, ile—ile sehemu ya kalisi na cho chote kinachoingia ndani yake, huijenga moja kwa moja zinapoingia katika hiyo punje, wakati jua linapoongezeka ukali.

65 Lakini ukichukua jua linalowaka Agosti, na kuliweka kwenye ngano leo, lingeiua. Hakika, huwezi kufanya jambo hilo. Halina budi kuja katika msimu wake. Vivyo hivyo na ngano ya Mungu na punje huiva tu katika msimu wake, msimu wa hiyo ngano. Lakini jua lingewezaje. . . Vema, ngano ingekufa, matunda yangekufa, kwa jua linaloishi leo, jua linalowaka leo, hasa. Mavuno yake yajayo yanaikomaza. Punje inapaswa kukomaa kulingana na hiyo nuru.

66 Lakini jambo lenyewe ni kwamba, siku hizi, punje ya kanisa haitaki kukomaa. Inataka kukaa kama ilivyokuwa huko nyuma katika wakati wa Moody, Sankey, Finney, Knox, Calvin. Wao walikuwa wako sahihi, walikuwa ndio nuru ya wakati huo.

67 Lakini hii ni saa nyingine. Hii ni siku nyingine. Huku ni kusonga mbele kwa Injili; inafikia kukomaa kwake. Kwa hiyo hatuwezi kuishi katika yale Luther aliyosema, Wesley aliyosema, ama baadhi ya hao wengine. Tunaishi katika Nuru iliyotabiriwa kwa ajili ya siku hii. Tuko katika Wakati wa Saba wa Kanisa, si wakati wa tatu ama wa nne wa kanisa. Punje inapaswa kuweza kulipokea Hilo. Isipolipokea, inaanguka wala haina maana kwake. Punje inakomaa kulingana na Nuru kama inasonga mbele pamoja na Nuru.

68 Vivyo hivyo na kanisa nalo linapaswa kuleta chakula cha kila wakati, ambacho Yesu aliamuru, ya kwamba, "Mtu ataishi kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu."

69 Chakula tunachohitaji kiko katika Biblia. Ni ufunuo mzima wa mpango wa Mungu. Ni ufunuo mzima wa Yesu Kristo. Hatuongezi lo lote Kwake, wala kuondoa lo lote kwake; kila afanyaye hivyo, jina lake litaondolewa kutoka katika Kitabu cha Uzima. Hatuhitaji kanuni zo zote kuongezea kwa hili. Limeandikwa namna ile ile hasa ambavyo linapaswa kuwa. Hatuongezei kitu cho chote Kwake, hatutoi lo lote Kwake, tunalihubiri vile vile tu lilivyo, Mungu ni, atalidhihirisha. Kila ahadi aliyoahidi, Yeye ataidhihirisha vivyo hivyo ilivyo. Hatupaswi kuondoa Kwake wala kuongeza Kwake. Liache tu jinsi lilivyo.

70 Lakini, unaona, siku hizi, tunaona watu kwa namna fulani kama vile ilivyokuwa katika siku zilizopita, wakijitahidi kuishi katika siku za nyuma katika mazigazi. Kanisa linapaswa kukomaa kwa mfano wa vile ngano inavyokomaa, "mtu huyo ataishi si kwa mkate tu, bali kwa kila Neno la Mungu, Mkate wa Uzima." Si sehemu tu ya Maneno; kila Neno la Mungu, kila wakati! Usikae tu na kula maharagwe na viazi wakati wote. Kuna mambo mengine yanayoambatana nalo, tunaposonga kuingia kwenye sehemu kamili ya mlo wa Chakula kikuu cha Mungu kilichoandaliwa mbele ya watu Wake, nguvu za Roho Mtakatifu, ku—kule kukifurahia, kutokana na nguvu na Roho ambaye ametolewa. "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya. Kwa kuwa mimi ni hai, nanyi pia mko hai." Ahadi ambazo Yesu alizitoa kwa kanisa Lake, na hata hivyo leo tunaona watu wakijaribu kurudi huko nyuma kabisa katika wakati mwingine uliopita.

71 Wakati wa Luther, ulikuwa ni wakati mkuu. Aliona kosa la kanisa Katoliki, aliona ushirika. Huyo, huyo kasisi kijana, aliona ya kwamba jambo hilo lilikuwa ni kosa, "haukuwa ni mwili wenyewe wa Kristo," ulikuwa ni kipande cha mkate ambacho—

ambacho walikuwa wamekibariki. Naye aliona ya kwamba, "divai hiyo haikuwa ni Damu yenyewe halisi," bali iliiwakilisha ile Damu. Kwa hiyo alikipinga kitu hicho kwa sababu majira ya wakati huo yalikuwa yamewadia. Na haidhuru walikuwa na makuhani wangapi, na cho chote kile zaidi walichokuwa nacho, Mungu alimpata mtu ambaye angeweza kuifanya hiyo nuru iangaze. Amina. Alikubali, "Kuhesabiwa haki kwa imani," naye aliifanya nuru ya wakati wa Luther kuangaza. Baada ya huyo kuja, kipindi hicho kilimaliza wakati wake.

72 Kulikuja wakati mwingine ambapo kanisa lilipaswa kuondokana na dhambi zake, na litakaswe. Akaja John Wesley, maskini mtu mdogo Mwanglikana kutoka huko Uingereza, aliyekuwa mfuasi wa kanisa la Anglikana, bali aliona nuru kwenye Injili. Ilikuwa ni saa ya ule Wakati wa Filadelfia kutokea. Na alipokuja, alihubiri kazi za pili za neema, utakaso kwa Damu ya Yesu Kristo. Hakuna kitu cho chote kiliweza kusimama katika nuru yake. Yeye alihesabiwa kuwa mshupavu wa dini kama vile tu Luther alivyochukuliwa, bali alipinga vile hao wengine wote walivyohubiri, na akaangaza nuru hiyo, kwa maana ilikuwa ndiyo nuru ya saa hiyo. Mungu alipata mtu, John Wesley, aliyeweza kuiwasha taa.

Alikuta kwenye ninii. . .na pia Luther, aliyeiwasha taa ya wakati huo.

73 Baadaye moja kwa moja wakaja ndugu wa Kipentekoste. Walirudi katika wakati wao, wa kurudishwa kwa vipawa, kurudisha vipawa, vya kunena kwa lugha, karama za uponyaji, na mambo kadha wa kadha kwa kanisa. Sasa, wao walifanya vile hasa Maandiko yalivyosema wangefanya, na, walipofanya hivyo, walidhihirisha jambo hilo. Hiyo ni kweli kabisa.

74 Lakini je! ulitambua ya kwamba tumesonga mbele zaidi kutoka hapo? Tuko katika wakati wa Bibi-arusi, wakati wa kuchaguliwa, wakati ambapo (Bibi-arusi) wao walisema tungekuwa nao. "Yote yaliyosazwa na madumadu," kasema Yoeli 2:28, "yote yaliyosazwa na madumadu, tu—tunutu wamekula; na yote yaliyosazwa na tunutu, nzige wamekula."

75 Kila moja ya hayo madhehebu, kama umesoma Mihuri Saba ya Biblia, kila mmoja wa hao watengenezaji alitoka akaenda na kuhubiri Neno, lakini aliacha kitu fulani. Halafu walifanya nini baada ya watengenezaji kukoma, na nuru ilianza kufifia? Badala ya kuendelea kuingia katika Nuru zaidi, waliiundia madhehebu. Na walipounda madhehebu, "Tunaamini Nuru *hii*. *Hii* ndiyo Nuru! *Hii* Ndiyo." Walifanya nini? Wesley alikuja moja kwa moja na akawatoka.

76 Wesley alifanya nini? Aliunda madhehebu yake, na nanii yake—ndugu yake, John na—na Charles, baadaye moja kwa moja akaja Asbury na hao, na, baada ya siku zao, waliunda madhehebu yaliyoitwa kanisa la Kimethodisti. Walifanya nini?

Walikataa Nuru ya zaidi. Walisema tu, "*Hii* ndiyo Nuru. *Hii* Ndiyo."

77 Ndipo wakaja Wapentekoste moja kwa moja na kuwaonyesha, ya kwamba Mungu angali anashusha ubatizo wa Roho Mtakatifu. Angali anashusha nguvu Zake za uponyaji, ambazo wamezikana. Walifanya nini? Wakatoka kwao moja kwa moja, kwa kuwa ilikuwa ni nuru nyingine?

78 Ni kitu gani sasa? Tumepita miaka kama sitini, Wapentekoste wameunda madhehebu, "Sisi ni *hili*, sisi ni *lile*," naye Mungu ameondoka moja kwa moja toka hilo; yuko huko nje, na anamleta Bibi-arusi, Mteule, kutoka kwenye kundi hilo. Ambapo, kamwe hakutakuwako na wakati mwingine wa kanisa. Wakati wa Kanisa la Filadelfia ulikuwa ni Wesley. Na Wakati wa Kanisa la Laodikia ni madhehebu ya Kipentekoste, ambayo yote yanaingia moja kwa moja katika alama ya mnyama. Hiyo ni Biblia, kama vile ambavyo ndugu huyu alikuwa akisema muda mchache uliopita. Hiyo ni kweli. Naam. Hayo ni ninii, hayo yote ni madhehebu, kwa sababu walikataa kutembea katika Nuru ya zaidi. Wanajiundia madhehebu, na wanasema, "Tunaamini jambo hili." Mungu anapofanya jambo fulani, lichunguze kwa Maandiko.

79 Mafarisayo walisema, "Tunalo." Masadukayo walisema, "Tunalo." Lakini Mungu alikuwa Nalo! Mungu amefungua na kuonyesha Nuru. Ilikataliwa kama daima ilivyokataliwa.

80 Kanisa Katoliki lilimkataa Luther. Wesley alimkataa Luther. Na vivyo hiyo pia Wapentekoste walimkataa Wesley.

81 Na Roho Mtakatifu leo anawakataa Wapentekoste. Mnakuwa wa kawaida tu na baridi kama hao wengine. Kila mtu anaweza kuona jambo hilo. Ninawapenda. Ninyi ndio kitu kilicho karibu sana na Biblia kuliko wote, nijuavyo, hiyo ndio sababu mimi niko pamoja na ninyi. Lakini, sikilizeni, fungueni macho yenu na mwone siku tunayoishi! Ni wakati wa ufunguo kufungua tena, na Nuru kuja, na kuuleta Mti. Biblia ilisema, katika Malaki 4, "Yeye angetuma na kurejesha tena Imani ya asili wailiyokuwa nayo watu." Yeye aliahidi jambo hilo. Amefanya hivyo daima. Alituma Neno Lake, nao manabii walikuja kwa sababu Neno liliwajia manabii, nao walikuwa na Neno na wakalifanya kuwa hai.

82 Madhehebu na mifumo ya wakati huo iliwakataa, kila wakati, kwa hiyo watafanya vivyo hivyo leo. Mungu anaweza kabisa hata leo hii kumwinua mtu wakati huu kama alivyoweza wakati uliopita. Yeye kamwe hakuinua madhehebu. Mwulize mwanahistoria ye yote, angalia katika historia; wakati shirika lilipojiundia madhehebu, lilifia hapo wala halikuinuka tena. Mungu huzungumza na watu binafsi. Kweli.

83 Naye Mungu aliahidi kufanya jambo hilo tena katika siku za mwisho, na kwamba atafanya hivyo. Yale Mungu ameahidi, hayo

atayafanya, kuiwasha taa inayoweza kuthibitisha Maandiko yaliyoahidiwa ya leo hii. Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za—za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu." Unaonyesha, unaona vile wanavyofanya. Mwangalie Yehova, yale amefanya, Baba yetu ameweka kila kitu mahali pake.

84 Kuna Lutu kule chini ulimwenguni, kule chini Sodoma, wenye kila dhambi, vuguvugu. Kuna mjumbe kule akimhubiria, pia.

85 Kuna kundi la Ibrahimu, Wateule, waliotolewa, wale walio na ahadi, wakimngojea Mwana kwa moyo wote. Lutu alikuwa akimtazamia mwana, pia, bali si katika hali ambayo Ibrahimu alikuwa akimtazamia. Ni kitu gani kilitukia? Kabla tu jambo hilo halijatukia, Mungu alishuka na kujidhihirisha Mwenyewe katika mwili, na kutangaza ya kwamba Yeye alikuwa ni lile Neno, kwa kuwa, "Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, na tambuzi la mawazo na makusudi ya moyoni." Yesu alisema, "Ndivyo itakavyokuwa tena, katika wakati wa kuja Kwake Mwana wa Adamu." Ahadi hizi ni za Kiungu, zilinenwa kwa mdomo wa Yesu Kristo. Mbingu na nchi zitashindwa, bali Hizo hazitashindwa kamwe. Mungu angali anaweza kutoka katika mawe kumwinulia Ibrahimu watoto. Loo, naam!

86 Tuko safarini mwetu, tuko kitu kama vile Israeli walivyokuwa. Israeli, katika safari yao, ilibidi wapate mana mpya kila siku, kwa kuwa mana mpya ilianguka. Hatupaswi kuishi katika nuru ya Luther, kuishi katika nuru ya—ya Wesley, ama kuishi katika nuru ya Pentekoste. Tuko katika kipindi kingine, Mana mpya.

87 Nini kilitukia kama walijaribu kuiweka mana hiyo hadi kesho yake? Ilipata mabuu. Ingewaua. Hiyo ndiyo sababu tuna wengi sana waliokufa kiroho, wanaojiita Wakristo. Wanakula mweko wa siku zilizopita. Wanakula mana ambayo tayari ina mabuu. Ni kama tu vile kapi lilivyo kwenye ngano, kama haitaingia kwenye ngano, inaondoka kwenye ngano. Na wakati Nuru inapokataliwa, hakuna ila jambo moja tu la kufanya, watu kugeukia giza. Sehemu yo yote ya usiku, ambayo ingekataa kuona Nuru, inarudi kuingia katika giza. Na vivyo hivyo ndivyo ilivyo katika Injili pia, katika kila wakati imethibitishwa kuwa hivyo. Tunaishi katika wakati huo.

88 Mana ya jana imeharibika. Ninawasikia watu wakisema "Miaka arobaini iliyopita, nilifanya *hivi* na *vile*." Hiyo ni kweli, bali ni vipi leo? Vipi kuhusu kanisa kuwaka moto kwelikweli? Tunazungumza kuhusu ya jana, vipi kuhusu kanisa leo? Na wewe kama mtu binafsi leo ni vipi? Kwa kuwa, ya jana hayatafaa kwa leo. Ilikuwa ni sawa jana.

89 Ujumbe wa Luther ulikuwa ndiyo nuru ya wakati huo, kama vile wa Yohana ulivyokuwa, bali kulizuka nuru kuu

zaidi. Vivyo hivyo na Luther naye alikuwa ni nuru kuu, nasi tulimfurahia kwa muda, bali ilikuja nuru nyingine iliyoizima yake. Kile ilichopaswa kufanya ilikuwa ni kuchanganyika na Hiyo mpya; nayo iliendelea ikawa Mkate kamili, ikaendelea ikawa Mana kamili ya Mungu. Bali wao walifanya nini? Waliunda madhehebu. Mwanadamu ameingilia hilo. Badala ya Mungu kuliongoza, mwanadamu na mifumo yake aliliingilia, akalipofusha.

90 Loo, Mti huu wa Bibi-arusi leo, umepogolewa. Tawi lo lote lisilozaa matunda linakatwa. Yesu alisema hivyo, Yohana Mtakatifu 15. Ni kitu kilichotendeka sasa, tunaona ya kwamba yamekatwa, yamepogolewa.

91 Kumbuka, moyo wenyewe hasa wa mti uko katikati ya mti. Tunda litaiva daima, sehemu ya mwisho ambapo mti utazaa tunda, ni moja kwa moja kwenye kilele chake, kwa maana hapo ndipo palipo na ubichi unaotoka katikati ya uhai ulio ndani ya mbegu.

92 Ni Mti wa Bibi-arusi. Yesu alikuwa ni Bibi-arusi, Yeye alikuwa ni Mti. Walimkata. Alikuwa ndiye Mti wa Uzima uliokuwa katika bustani ya Edeni. Walimkata na kumsulibisha juu ya mti wa Kirumi, wapate kumdhihaki. Yeye alifanya nini? Mungu alimfufua katika siku ya tatu, kutoka kwa wafu. Na leo kuna Mti wa Bibi-arusi; ulianza huko nyuma hapo mwanzo, huko nyuma kabisa katika Siku ya Pentekoste.

93 Sikilizeni, ninyi watu ambao ni washiriki wa kanisa! Kanisa kamwe halikuanzia huko Nikea, Rumi. Lilianzia huko Yerusalemu, kwenye Siku ya Pentekoste, kanisa lilianza. Ndipo walifanya nini? Waliendelea tu kuunda madhehebu; na Mungu anaendelea kukata matawi. Ndipo wakaunda la Kilutheri; akakata matawi. Wesley; akakata matawi. Pentekoste; akakata matawi. Mpaka imefikia . . .

94 Lakini Mungu atakuwa na Mti wa Bibi-arusi! "Yote yaliyoliwa na parare na madumadu wamekula, nitayarudisha," asema Bwana. Malaki 4 inatwambia tutarudishwa kwenye Imani ya mwanzoni kama ilivyokuwa kwenye Siku ya Pentekoste, "Imani ya baba." Tunaamini kwamba itakuja. Ninaamini wakati wake umewadia sasa. Matawi yamenyauka na kukauka, nao watayaondoa kwenye ule Mti, ili kwamba matunda yaweze kutunga moja kwa moja juu kileleni kabisa mwa Mti. Loo, jamani!

95 Nuru hizi zote ni sawa. Kanisa leo ni hiyo nuru pamoja na yale liliyopokea leo. Linapaswa kumalizia wakati wa mavuno. Kama tunavyoona, ya kwamba Mti huo wenyewe, ama . . . Ngano haina budi kukomaa kuendana na hiyo Nuru, ikikua kutoka kwenye jani hadi kwenye punje, na kutoka kwenye punje na kuendelea. Inakomaa sambamba na Nuru. Nuru ya nyakati zingine zinaushuhudia tu wakati huu. Nuru ya Luther

ilishuhudia nuru ya—ya Wesley. Wesley alishuhudia nuru ya Pentekoste. Ni nuru ile ile, inaivishwa tu na ile Nuru. Laiti watu wangaliweza tu kuona jambo hilo!

96 Muda fulani uliopita, nilikuwa nikisoma makala mafupi, ambapo malkia wa Uingereza, (si malkia huyu) malkia yule mwingine, alienda kuona kampuni ya karatasi iliyokuwa ikitengeneza karatasi nzuri sana. Na wakati alipozungumza na rais wa kampuni hiyo, alimtembeza. Alitaka kuona jinsi ambavyo karatasi hiyo nzuri ilivyotengenezwa. Alimpeleka na kumwonyesha mitambo yote mikubwa ya kuchapishia na kadhalika. Na katika siku hizo, walitengeneza makaratasi kutokana na matambara ya nguo. Tunakumbuka vema jambo hilo. Kwa hiyo huyo rais aliingia kwenye chumba fulani na kufungua mlango, wala hakukuwa na kitu ila tita la matambara. Malikia, kwa mshangao mkubwa, alisema, "Vitu hivi vichafu vina kazi gani?"

97 Mtu huyo, ambaye alikuwa ndiye rais wa kampuni hiyo, akasema, "Vitu hivyo vilikuwa ni nguo, hivi karibuni. Unaona, zimekuwa ni chafu. Hatuzitupi, bali ndizo karatasi za kesho."

Akasema, "Sielewi na jambo hili."

Akasema, "Utalifahamu kesho."

98 Kwa hiyo walipoyapitisha matambara haya katika mtambo wa kuchapisha, kupitia mchakato wa kusafisha, na—na kitu fulani ilichopaswa kupitia, mchakato; wakati yalipotoka, yalikuwa ni karatasi nzuri sana. Huyo rais alifikiri angemwonyesha malkia kitu fulani ambacho hajawahi kujua. Aliweka picha ya malkia katika hiyo karatasi, na kuisindika katika karatasi hii nzuri. Wakati malkia alipoipokea hiyo karatasi, aliona sura yake mwenyewe katika yale yaliyokuwa ni matambara machafu, jana, kwa sababu yalipitia katika mchakato fulani.

99 Loo, kama Luther, Wesley, na hao wote, wangeweza kuona jambo hilo, ya kwamba hayo mahubiri ya jana yanaweza tu kutumiwa kama yakipitishwa katika mchakato fulani! Wakati Roho Mtakatifu anapoifunua Nuru, kutoka kuhesabiwa haki hadi utakaso, hadi ubatizo wa Roho Mtakatifu, na sasa saa ya mwisho ya kule Kuja kwa Kristo; ina sura ndani yake, si ya malkia, bali ya Mfalme wa Mbinguni anayejiwakilisha Mwenyewe, kwa kuwa kanisa limekaribia kuingia kwenye uchache, kama ambavyo hiyo huduma haina budi kuwa ni aina ya huduma kama ile ile aliyokuwa nayo.

100 Wale waliokufa katika wakati wa Luther, kule chini ya piramidi, kitu kama hicho; si mafundisho ya piramidi, bali ni kwa mfano tu.

101 Hilo piramidi ni kamilifu sana, kama ye yote wenu amepata kuwako kule. Huwezi kupitisha wembe, ni vigumu. Ninii—hawakuweka mota humo, kadiri tujuavyo sisi. Ufundi wake wa

ujenzi ulikuwa ni mkubwa sana! Sasa, walilipoteza lile jiwe la juu. Hawajui liko wapi. Sasa wakati jiwe hilo la kuwekwa juu litakaporudi, litakuwa tu ni kama hayo mengine, litaunganika na lile jiwe lililoachwa wazi. Kama ungeweka jiwe la kichwani juu yake, itabidi liwe hivyo.

102 Na wakati Yesu atakaporudi, atakuta Kanisa lililooshwa, lisilo na waa wala kunyanzi, na itakuwa ni huduma ile ile aliyokuwa nayo. Itarudisha Jiwe la Juu.

103 Kama vile mkono wangu hapa, katika kivuli. Ni kivuli, ila tu ni mweusi zaidi mkono wangu unapokuwa ninii zaidi... Ni kivuli *hapa*, halisi *hapa*. Kama negativu na halisi, unakuwa mzito zaidi; mweusi zaidi, mweusi zaidi, mweusi zaidi, na hatimaye unashikamana pamoja, na negativu na halisi inakuwa ni kitu kimoja.

104 Hapo ndipo Kanisa na Kristo wanapoungana pamoja, kama Bibi-arusi, likiwa na Roho yeye yule aliyekuwa ndani Yake atakuwa juu ya Bibi-arusi; wakati Kanisa hilo linapokuja kutoka kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, mpaka kwenye siku za mwisho, na kulichonga sasa kwa ajili ya kule Kuja kwa Bwana.

105 Loo, usiwe kwenye mahali pake panapokuparuza, ewe ndugu Mpenkoste. Ung'are kwa Neno na uamini kila chembe Yake ndogo. Usitoke ukaingia katika hizi itikadi na mambo kadha wa kadha, kama vile tunavyoziona hizo zikiendelea siku hizi. Usishangazwe na jambo hilo, kwa kuwa Jiwe la Kichwani linakuja, likilia, "Aba, Baba," hivi karibuni sana, "Mungu Wangu! Mungu Wangu!" Naam, ninaamini jambo hilo kwa moyo wangu wote.

106 Je! mnaliona? Mnajua ninalomaanisha? Ni Kristo sasa akichukua matambara ya jana, ya Kilutheri, Kimethodisti, Kipresbiteri, na kadhalika, naye anayapitisha katika mchakato. Ni mchakato wa namna gani? mchakato wa Roho Mtakatifu; kile walichokuwa nacho, na zaidi; akikiumba mpaka Yeye anasindika sura Yake Mwenyewe, wakati Kanisa na Kristo wanakuwa mmoja katika muungano. Mungu, tujalie! Ninatumaini ya kwamba mnaona jambo hilo. Kama mnaliona...

107 Inanikumbusha hadithi moja, ambapo wakati ule—ule uamsho mkuu wa Kiwelshi ulipokuwa ukiendelea. Watu fulani wakuu hapa nchini walikusudia ya kwamba wangeenda kule na waone uamsho wa Kiwelshi, kile kingekuwa kinaendelea. Na walipofika kule, wapate kujua, waone ni kwenye jengo gani ulikuwa ukiendeshwa. Walipofika Wales, walizunguka-zunguka, wakaanzia kuulizia mahali jengo hilo lilipokuwa. Walimwona maskini afisa mmoja mwenye furaha amesimama pembeni, amevaa kofia yake ndogo iliyolegea, naye alikuwa akizungusha-zungusha kirungu chake namna hiyo. Na kwa

hiyo watu hawa walimwendea, na kusema, “Bwana, ungeweza kuniambia ufufuo wa Kiwelshi unafanyikia kwenye jengo lipi?”

108 Akasema, “Naam, bwana, mimi ndio huo! Mimi ndimi huo!” Kwa nini? Alikuwa akiangaza furaha pamoja na Nuru ya Kiwelshi—uamsho wa Kiwelshi ndani yake.

109 Vivyo hivyo na kanisa la Kipentekoste linapaswa leo, linauliza, “Yesu Kristo ni nani? Yeye yule jana, leo, na hata milele!” Nuru Yake ya Injili Yake inapaswa kuwa inaangaza pamoja na Neno la wakati huu, ikimfunua Yesu Kristo kwa taifa, kama tu ilivyokuwa wakati huo.

110 Yeye alikuwa amejazwa sana na ufufuo wa Kiwelshi mpaka alikuwa ndiye ufufuo wa Kiwelshi.

111 Tunapaswa kujazwa sana na Kristo mpaka tu—tumwakisi Yeye katika nguvu za Neno Lake tulilogawiwa kwa siku hii. Enyi ndugu, msizamie katika mambo ya dunia, msizamie, shughuli hizi zinazowakengeua. Dumuni na Injili. Iweni makini na kila Neno! Msirejee nyuma kwa yale baba fulani aliyosema. Hebu twendeni sasa hivi kwenye yale Yesu aliyosema yatatukia katika siku hii. Naam, bwana. Tunapaswa kuwa Nuru ya wakati huu, tukidhihirisha Injili. Luther alikuwa ni nuru yake. Wesley na nuru yake, Pentekoste ilikuwa ni nuru yake. Lakini, tumepanda kwenda mbali zaidi barabarani sasa, tunaingia katika Bibi-arusi, walioitwa, Walioteuliwa. Kumbukeni, kama wewe ni ninii, wewe ni kama tu yule afisa, yeye alikuwa Nao ndani yake.

112 Kumbukeni, huu ni wakati wa saba wa kanisa, Wakati wa Kanisa la Laodikia. Kulingana na Ufunuo 3, wanamkataa Kristo. Kwa kila wakati wa kanisa uliotajwa katika Biblia, Wakati wa Laodikia ulikuwa ndio mbaya kabisa wa hizo zote. Ulimtoa nje, ulimkataa, ukamtupa nje.

113 Je! uliona mwezi ukiingia giza kabisa, hivi majuzi usiku, kabla ya papa kwenda huko Roma, kutoka Roma kwenda Yerusalemu? Yerusalemu, kanisa la zamani kuliko yote; mwezi ni mfano wa kanisa, daima ukiakisi nuru ya jua, jua lisipokuwapo, nao uliingia giza kabisa. Nilichora hayo kwenye ubao hapa, miaka mitatu ama minne iliyopita, na kuonyesha makanisa, katika mamia na maelfu ya makazi kote nchini. Ilikuwa ni kitu gani? Kivuli. Mara ya kwanza ambapo papa aliwahi kuondoka, kurudi hapa, akaja katika—katika jina la Paulo, na kadhalika, akashuka akapitia sehemu zile; ilibidi abariki mto, ili kuuvuka, na kadhalika. Mto unaninii—mto unahitaji baraka za nini?

114 Hivi wakati huu wa kanisa tunaoishi leo una shida gani? Hivi hamwezi kuona jambo hilo? Mungu akilitangaza jambo hilo huko juu, akilitangaza katika Neno Lake, akilitangaza katika gazeti, akilitangaza miongoni mwa watu? Hivi hamwezi kuyafungua macho yenu na kuuona wakati huu? Haya ndiyo yanayoshuhudia hiyo Kweli. Hii ndiyo Nuru ya saa hii.

115 Angalieni huo uamsho mkuu wa ekumeni, unaingia katika halmashauri hii kule sasa, ukifanya tu sanamu ya mnyama, katika Ufunuo 17, vile vile hasa lilivyosemwa utafanya. Je! ninyi Wapentekoste mtalinyamazia jambo hilo na kuingia ndani yake? Ile saa ya kulazimisha imewadia.

116 Sasa huu ndio wakati wa kusimama na kutengeneza taa yako, na kuangaza kwa Injili ya Yesu Kristo na Nguvu Zake.

117 Ninajua hili halipendwi na watu wengi, wakati marafiki wangu wengi wa Kipentekoste walipoketi na papa na kadhalika, na kusema, "Ni hisia ya kiroho sana." Kwangu mimi, ni—ni makosa. Ni kinyume na Biblia. Hebu Neno la Mungu na liwe Kweli. Naam, bwana. Wakati umewadia sasa. Tunaona mabadiliko haya makubwa yakiendelea katika . . . Loo, linaonekana ni zuri kwa jicho la kawaida, hakika.

118 Kayafa alionekana ni mzuri kwa yale aliyokuwa akiwafunulia hao makuhani, katika siku ile, siku yote hiyo nzima. Lakini Yesu alikuwa ndiye Nuru iliyokuwa ikilifanya hilo Neno liishi, bali halmashauri zao na kadhalika zilikuwa zimeyapofusha macho yao kwa Hilo. Yeye alisema, "Waache; kipofu akimwongoza kipofu mwenzake, wote wataanguka shimoni."

119 Tumerudi kwenye wakati huo tena, ndugu na dada. Tumerudi kwenye wakati huo tena. Angalia. Kwa nini? Sababu ile ile.

120 Tunaona ya kwamba ninii—nuru hizi kuu ambazo tuliishi ndani yake, katika siku zilizopita, zilikuwa ni sawa, hatuna kitu dhidi ya hizo. Lakini, Wakati huu wa Kanisa la Laodikia, iweni waangalifu, kumbukeni, ni uliomkataa Kristo. Na hivyo ndivyo ilivyo hasa sasa.

121 Halmashauri hii kuu imeenda kote, kuwaunganisha Waprotestanti wote pamoja, uvuvio huu wa ekumeni. Nao unafanya nini? Unalitia giza Neno halisi, lenyewe, nalo Neno ni Kristo. Wanawezaje kufanya jambo hilo? Wakati, Wakristo wa Kisayansi, na Muungano wa Ndugu, na wengi wa hao watu katika madhehebu mengine makubwa, wengine wanaamini kuzaliwa kibikira, wengine hawaamini, wengine wanaamini *hivi* na *vile*. Unawezaje kujiunga na kutokuamini? "Watu wawili wanawezaje kutembea pamoja wasipokuwa wamepatana?" Tokeni kati yao mkatengwe nao, na mchukue Neno Takatifu la Mungu na mdumu Nalo.

122 Yesu Kristo anawajibika kulidhihirisha Neno Lake. Jambo tunalohitaji siku hizi ni kuinuka kwa Malaki 4. Nabii mwingine atainuka katika Jina la Bwana Yesu Kristo, naye ataleta kile hasa Yeye alichoahidi kufanya. Ndipo, mtu atalikataa bila kujua na kuingia moja kwa moja gizani, kama vile wamefanya daima.

123 Angalia sasa, tunaona, sababu ile ile, ya kwamba leo, kwamba wanakataa, makanisa yanakataa Ujumbe,

yanalisulibisha Neno, wanaondoa Neno. Sasa kama wewe si wa hilo, huwezi hata—huwezi hata kuhudhuria kanisa lako. Watalifunga. Inakulazimu kuingia ndani yake. Usipoingia, unafungiwa. Basi ni vipi kuhusu hilo? Loo, shindania Hilo lililo kweli! Kumbuka, ni wakati wa kusulibishwa tena, umekaribia.

124 Nuru ya bandia ilisababisha unyang'anyi mkubwa—mkubwa kuliko wote ambao dunia iliwahi kufanyiwa, huko Uingereza, si muda mrefu uliopita. Unyang'anyi mkubwa sana uliopata kufanywa, ulifanywa kwa nuru bandia. Unyang'anyi wa dola milioni saba ulifanywa kwa nuru ya bandia iliyofanya hilo garimoshi lipunguze mwendo, wala Scotland Yard haikuweza kumpata mtu huyo. Walitoweka nazo, wajanja sana. Huo ulijulikana kama unyang'anyi ulio mkubwa kabisa uliopata kufanywa na wanyang'anyi, katika mambo ya maumbile ya kawaida. Iliuibia ulimwengu, unyang'anyi wake ulio mkubwa kuliko wote.

125 Na unyang'anyi mkubwa sana uliowahi kufanyiwa kanisa la Yesu Kristo, unafanywa na nuru bandia, mweko wa wakati fulani mwingine, na kuikataa Nuru ambayo imetabiriwa kwa ajili ya wakati huu. Amina. Nuru ya bandia, mweko wa jana! Usitembee katika mweko wa jana. Tembea katika joto la Mwana leo. Usijivute kujiingiza katika kivuli cha kimadhehebu, ukisema, "Siku za miujiza zimepita."

126 Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: katika Jina Langu watatoa pepo, watasema kwa lugha mpya. Ishara hizi zitafuatana na hao."

127 Wao husema, "Ni sawa kwa mitume; si kwetu sisi." Hayo ni mazigazi.

128 Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, ulimwenguni kote." Naam, bwana.

129 Sasa kuna shida gani? Kutembea katika mweko, kumesababisha wizi ulio mkubwa kuliko wote, kumemwondoa Kristo kanisani. Unaona, Kristo anawezaje kujidhihirisha katika Neno lililoahidiwa leo, kwa kanuni fulani baridi ya jana? Haipashi mbegu joto. La, bwana. Wizi ulio mkubwa sana wa kanisa!

130 Ati joto? Na, kumbukeni, nuru hiyo baridi ya kanuni ya imani haitaiivisha Mbegu ya leo. Inaikana hiyo Mbegu. Hiyo ni ukungu ulio juu ya dunia, utusitusi. Wakati umewadia wa Mungu kuamka na kuiwasha Taa tena, kulifanya Neno Lake liishi. Hakika, Nuru! Kanuni hiyo baridi ya imani haitaiivisha hiyo Punje. Hakika haitaiivisha.

Na, kumbukeni, ustaarabu umesafiri pamoja na jua.

131 Kama nilivyowaambia pale mwanzo, sina budi kuangalia mifano, jinsi maumbile yanavyotenda. Sina elimu ya kufanya jambo hilo; siitaki. Ni afadhali niwe na kile nilicho nacho,

kuliko nipate elimu yote ya dunia. Nina Yesu Kristo. Ninamwona akiliishi Neno Lake kikamilifu kabisa, na hilo ndilo tu ninalohitaji kujua.

132 Na kama mtu amezaliwa na Roho wa Mungu, atayachunguza Maandiko aone kama ni jibu la siku hizi. Jibu la siku hii ni Kristo. Kristo ni Neno. Wakati Neno linapohuika, linaonyesha Nuru iliyoahidiwa kwa ajili ya siku hii. Wakati huu wenye giza wa Laodikia, ni wachache tu, "Wote ninaowapokea, ninawarudi, ninawakemea. Tubuni," Yesu alisema, "pia rudini." Ligeukieni Neno. Yeye ni Neno. Njoni Kwake. Naam, bwana.

133 Angalieni hiyo Nuru. Ilitoka Mashariki, ikienda magharibi. Tuko Pwani ya Magharibi. Ilikuwa ina hatua tatu, sivyo? Ilikuwa na hatua tatu. Ilivuka maji, mara tatu. Kutoka kwa Paulo, na kuvuka Mediterania, ikaingia Ujerumani, Ujerumani ikaangaza kwa Luther; ikavuka Mlangobahari wa Uingereza, ikaingia Marekani na sasa. . . ikaingia—ikaingia Uingereza; halafu, Uingereza, ikavuka Pasifiki, ikaingia Marekani. Na imepitia katika ujumbe wa Luther, ikaendelea moja kwa moja, mpaka sehemu Yake ya mwisho iko hapa kwenye Pwani ya Magharibi tena.

134 Na hiyo kutoka kwenye kuiva kwa hiyo punje, kutoka huko nyuma kabisa kwa Luther, huko nyuma kote katika nyakati, inapaswa kuwa ni ukamilifu wa Injili sasa, Nguvu za Mungu za kuivisha. Nuru ambayo imeonyeshwa kupitia kwenye kuhesabiwa haki, kutakaswa, wakati wa pentekoste, inapaswa kuuivisha Mti wa Bibi-arusi kwa ajili ya Kuja kwa Bwana Yesu Kristo; ili Kristo aweze kudhihirishwa katika Kanisa Lake, kama Mtu mmoja, Yeye na Mke Wake, Yeye na Bibi-arusi Wake. Amina. Hii ndiyo saa tunayoishi. Hii ndiyo Nuru ya siku hii. Tembeeni ndani Yake! "Okokeni, enyi miisho yote ya dunia."

135 Mweko wa kanisa wa siku hii ulikuwa ni mdanganyifu sana, Yesu alisema katika Mathayo 24. Yeye alisema, "Ingewapoteza walio wateule kama yamkini." Unaona, si kwamba Luther asingeipokea. . . Luther asingeweza kumdanganya Mmethodisti. Mmethodisti asingeweza kumdanganya Mpentekoste. Hiyo ni kweli, unaona, lakini vipi kuhusu Bibi-arusi? Hicho ndicho kinachoyapofusha macho ya Wapentekoste. Naam. Unaona, mlirudi kwenye kanuni yenu ya imani, kwenye utaratibu wenu, mkaunda madhehebu, na mkapata kundi la watu linalowaambia la kufanya.

136 Biblia inaahidi mambo haya. Tunahitaji wanaume na wanawake waliojazwa na Roho wa Mungu.

137 Kama ukisema una Roho wa Mungu ndani yako, na Mungu anafanya ahadi fulani Humu, huyo Roho Mtakatifu anawezaje kuiitikia, kusema, "Vema, huenda ikawa ni sawa kwa wakati mwingine. Sisi hatuliamini namna hiyo"? Huyo si Roho Mtakatifu.

138 Mtu aliyejazwa na Mungu, Yeye na Neno ni mmoja. Hakika, ndivyo ilivyo. Ni matokeo ya muungano, muungano kati ya Mungu na mwanadamu.

139 Mwanamke anawezaje, ambaye atakuwa ni mume wa mwanamume fulani, kinyume, kufanya mambo ambayo huyo mume hataki huyo mwanamke ayafanye? Tunawezaje kufanya ubembe na ulimwengu, na madhehebu na mashirika, na kuikataa Nuru ya saa hii? Inawezekanaje, ndugu na dada? Kwa upendo wa kiungu na heshima kwa kila mmoja wenu, tunawezaje kuyakubali mambo haya? Tunawezaje kuisikia? Linatupwa moja kwa moja kwenye paja letu tena.

140 Msiwahukumu Walutheri; kwa sababu, walihukumu Katoliki. Msimhukumu Wesley; kwa sababu, alimhukumu Mlutheri. Unaona, namna hiyo, wakati mnapohukumu Jambo hilo linalotendeka leo na kulipa kisogo; wakati mnapoona makanisa yenu yakiingia katika uvuvio huu mkuu wa ekumeni, na kadhalika namna hiyo, yakiwaongoza, kila mmoja, kuwaingiza katika alama ya mnyama, nanyi mnayo. Watu wengi wenye mioyo minyofu wanaenda na kuingia moja kwa moja humo.

Unasema, "Hao ni watu wazuri, watu watakatifu."

141 Ndivyo ilivyokuwa kwa hao makuhani. Kama ingalinibidi kuchukua utakatifu wa Yesu Kristo, ama matunda ya Roho, wengi wenu mmepitia haya . . . Sasa, si kupuuza jambo hilo. Ninaamini kila Neno lake.

142 Wengi watasema, "Loo, nilinena kwa lugha. Nimempata." Huyo siye. La, bwana.

Wengi wao wanasema, "Tunda la Roho, huyo Ndiye." Ni kweli?

143 Hebu na tumweke Yesu mahakamani (Mungu, nisamehe) kwa muda kidogo. Hebu na tukulete hapa, na mimi nitakuwa ni kuhani. Nitakwambia, "Kijana huyu, aliyeingia mjini, anayeitwa Yesu wa Nazareti. Msimsikilize. Sisi tunaamini tunda la Roho. Sasa hebu angalieni hapa, maskini kuhani wenu mwenye huruma. Yeye, babu yake, baba wa babu yake, wote walikuwa ni makuhani. Alijitolea, maisha yake yote ya ujana. Aliishi siku zote seminari. Alitunza, aliamini, a—alifanya kila kitu walichowahi kumfundisha. Anayafahamu Maandiko, kutoka A hadi Z. Hata anayaandika, yeye mwenyewe. Huyaandika Maandiko, yeye mwenyewe, waandishi huyaandika. Naye yuko hapa, mtu mzuri sana! Mnajua yeye ni mtu mzuri.

144 "Ilikuwaje wakati mama yako alipokuwa anakuzaa? Ni nani aliyesimama karibu na kitanda chako? Maskini kuhani huyo mzee mwenye huruma. Wakati mama na baba walipokuwa wakitaka kwenda kutengana, ni nani aliyewakumbatia wote wawili na kuwaongoza kuwarudisha kwa Mungu? Huyo maskini kasisi mwenye huruma. Naam.

145 "Na hapa Yehova anahitaji mwana-kondoo wa sadaka, kwa ajili ya dhambi. Wafanyabiashara, wanaishi hapa mijini nao—nao wanauza bidhaa zao, na—na kadhalika, bidhaa zao na mazao yao, na cho chote watakachouza. Hawafugi wana-kondoo. Na hao makuhani walifanya nini? Walitengeneza kibanda kidogo kule juu, kusudi wapate kuuza wana-kondoo, kusudi mtu huyu apate kuingia, aiweke sawa nafsi yake na Yehova.

146 "Jamaa huyu, Yesu wa Nazareti, alifanya nini? Alitoka kwenye kanisa gani? Yeye ni wa madhehebu gani? Ana kadi gani ya ushirika? Tutamfukuza. Hatutakuwa na uhusiano wo wote Naye, kwa sababu Yeye anatuhukumu kila mmoja wetu. Yeye alifanya nini? Anapanda kwenda kule na kuondosha hayo, ambapo watu wanajaribu kuziokoa nafsi zao, kanisa," kama ambavyo tungaliliita leo, ninyi watu wa kiroho, "Aliipindua meza, akatupa chenji nje; akachukua kamba na kuzisokota, na kuwafukuza nje; na kumwita huyo kuhani wenu mzee mcha Mungu, 'mwana wa ibilisi,' maskini huyo mzee mwema aliyewakopesha zile fedha mlipokuwa kwenye shida."

147 "Ni nani atakayekusimamia na kukuzika utakapokufa? Si ni maskini huyo kuhani mwenye huruma. Yeye ana tunda la Roho. Lakini je! huyu Yesu wa Nazareti ana tunda la Roho?"

148 Huwezi kupima kwa kunena kwa lugha, wala huwezi kupima kwa tunda la Roho. Bali ni dhihirisho la Neno la Mungu, lililodhihirishwa. Nuru ndiyo inayofanya jambo hilo.

Mtu anayetembea katika Nuru hiyo! Yesu Kristo hakuwa akiweka msingi juu ya kunena kwa lugha, ingawa alinena kwa lugha. Yeye hakuwa ni tunda la Roho, ingawa Yeye alikuwa hilo. Usingeweza kuliamua jambo hilo. Bali Yeye aliliamini na kuliitikia, Na Mungu aliishi kila Neno la ahadi la siku hiyo kupitia Kwake. Hiyo ndiyo Nuru ya wakati. Hilo ndilo thibitisho.

149 Wakati mtu anaponiambia ya kwamba Roho Mtakatifu anayewashukia hao atakana Neno la Mungu kwamba ni kweli, kuna kasoro na jambo hilo. Kuna kasoro fulani kwa seminari zetu, na kadhalika, wakati wanapomfundisha mtu thiolojia yote hii hapa iliyotiwa kasumba na upuuzi wa siku hii. Watu hao wangalifanya vivyo hivyo dhidi ya Neno la Mungu, na kuwaongoza moja kwa moja kule katika maangamizi ya ekumeni, kwa nini, bila shaka, ni makosa.

150 Ninanena hayo katika Jina la Bwana! Ninyi lingojeni mwone kama Hilo si kweli, hiyo Nuru, Nuru ya wakati huu!

151 Kanuni hizo baridi za imani haziwezi kamwe kuleta mavuno. Hatuna budi kuwa na Kanisa ambalo limeoshwa kwa Damu ya Mwana-Kondoo, na kuwa kitu kimoja na Neno, ili kuwa Kanisa.

152 Mieko ya siku hizi ya kanisa, Yesu alisema, inadanganya sana, "karibu walio Wateule kama yamkini." Wateule tu! "Lakini kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, wakati watu

wanane waliokolewa, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja Kwake Mwana wa Adamu." Ni wachache sana, sana watakaokolewa katika wakati huo.

153 Inafanya nini? Inaongoza moja kwa moja machinjioni. Tunaona hayo katika giza hili la sasa tunaoishi. Ninafunga, kwa kusema hivi. Katika giza hili la sasa tunamoishi, siku hizi ambazo tunaishi sasa, wakati Nuru tayari imezimwa mbinguni, imezimwa hapa miongoni, kabla, kutuonyesha; ilionyeshwa kwa Biblia, kwenye Mihuri Saba, kile kilichokuwa kikitukia. Na hapa Mungu anatangaza jambo hilo moja kwa moja mbinguni, anashuka moja kwa moja na kulitangaza duniani. Na makanisa yanaingia moja kwa moja katika kitu hicho!

154 Ni nani atakayemwokoa basi maskini huyo Bibi-arusi anayeshikilia Neno? Itakuwaje Kwake atakapotupwa huko nje kwenye baridi, akiwa peke Yake? Hatashikwa na baridi, Neno la ahadi lililothibitishwa la siku hii. Loo, naam. Ni kama ninii . . .

155 Linatatiza, ninajua linatatiza, kwa watu, kuona kanisa likisema tu, "Vema, karibu ni jambo lile lile tu." Yesu alisema ingekuwa hivyo. Ningekuwa, hata, "Ingewapoteza walio wateule kama yamkini." Loo, ndio. Ndio, bwana.

156 Inanikumbusha tu juu ya jamaa fulani huko Florida, si muda mrefu uliopita. Alikuwa akizungumza, alisema alikuwa na gari la Chevrolet lililomharibikia huko Florida, naye akasema alilipeleka gereji. Na huyu makanika alikuwa anapita pale, naye akatengeneza kila kitu, na hakuweza kulifanya liwake. Aliweka kila kitu ndani yake, alichoweza. Alivikarabati vitu hivi vyote mbalimbali, lakini, kwa namna fulani au nyingine, haikufaa kitu. Na hakuweza kulifanya liwake. Alikazana tu kujaribu na kujaribu. Maskini makanika huyo alikuwa na wasiwasi, alikimbia huku na huko, pande zote jengoni, akichukua hiki.

157 Na mtu aliyekuwa amesimama, anasema, "Ninangojea gari langu, bwana. Nimechelewa. Hivi huwezi kulitengeneza?"

158 Akasema, "Ninafanya yote niwezayo kufanya," akiwa na wasiwasi sana na kushughulika. Na huyo mtu akatembeatembea.

159 Mara mtu mmoja mwungwana aliyevalia vizuri akaenda pale na kumwangalia kwa dakika chache, ndipo akamwambia huyo makanika, baada ya kumwacha asumbuke kidogo, akasema, "Kwa nini usiguse tu hiki? Hupati umeme wo wote."

160 Kwa hiyo akasema, "Sikuwazia kamwe jambo hilo." Kwa hiyo alibonyeza tu kitu hicho kingine kidogo, cho chote kile kilichokuwa pale, naye akaingiza u—umeme, gari likawaka.

161 Aligeuka na kusema, "U nani wewe?" Unajua yeye alikuwa ni nani? Mhandisi mkuu wa—wa General Motor. Ndiye aliyekiunda kitu hicho. Ndiye aliyekibuni.

162 Katika saa hii, ndugu, wakati tunaposhangaa nini kimeupata uamsho wetu, kuna nini? Tuna nyenzo na kila kitu, tuna mitambo, bali je! iko wapi Dainamikia? Hiyo ndiyo tunayohitaji, kumleta Yesu Kristo jukwaani. Kuna shida gani? Nawaambia, yupo Mmoja hapa leo, haleluya, anayeitwa Roho Mtakatifu, ambaye anaweza kuigusa Dainamikia. Yeye ndiye Dainamikia ya hiyo mitambo.

163 Tunasimama leo, sisi Wapentekoste, moja ya makanisa yaliyo makubwa sana nchini, maelfu mara maelfu wanaongezeka kila mwaka, lakini huyo Roho Mtakatifu yuko wapi? Tumekubali jambo hilo, kwa kunena kwa lugha, na tumeona jinsi lilivyofanya. Methodisti hulikubali, kwa kupiga makelele. Luther alilikubali, kwa imani, na kadhalika namna hiyo. Huyo siye.

164 Ni Neno! Ni kuwashwa kwa Neno, Nuru inaiwasha mitambo nayo inakuwa Dainamikia. Hiyo ni Dainamikia, wakati Dainamikia, wakati Dainamikia inapoingia kwenye mtambo. Inaanzisha kitu hicho kuzunguka. Hiyo ni kweli. Chukua Neno. Kama kuna kitu kimoja kilichokosekana, Kwake, halitawaka. Weka kando kila mzigo, kila itikadi, kila kanuni ya imani, kusudi Dainamikia, Roho Mtakatifu, aweze kumiminika katika Neno na kulithibitsha Neno lililoahidiwa kwa ajili ya siku hii; ndipo Kanisa kuu la Mungu litasimama kwa miguu yake kama ndege inayoendeshwa na jeti, liruke kwenda hewani kumlaki Bwana wake. Hiyo ni kweli kabisa. Mpaka tutakapofanya jambo hilo, halitafanya kitu. Hivyo ndivyo ilivyo. Naam, bwana. Ni nani atakayefanya jambo hilo? Ni nani atakayelishikilia katika siku hii tunayowazia habari zake? Kumbuka, kumbuka, ewe ndugu.

165 Sasa inanikumbusha juu ya hadithi nyingine fupi. Si kurudi kwenye hadithi, lakini rafiki yangu mmoja alikuwa amesimama huko Carlsbad, New Mexico, wakati tulipokuwa kule tukifanya mkutano huko Carlsbad. Na kulikuwako na kundi la watu walioingia katika pango hili.

166 Loo, kamwe si—sikupenda jambo hilo, huko chini ambako ni kina, na yapata maili moja chini ya ardhi. Mimi, mimi nimeridhika huku juu. Kwa hiyo, waliingia ndani mpaka mwisho kabisa. Mimi ninataka kupanda juu zaidi, si kutelemka chini zaidi. Kwa hiyo ni-. . .

167 Walimchukua jamaa huyu, wakatelemka huko chini. Naye alikuwa rafiki mwanamume, na msichana wake mdogo pamoja na mvulana wake mdogo walitelemka pamoja nao. Na—nao wakaingia ndani kabisa katika chumba cha chini, loo, nadhani, mamia na mamia na mamia ya futi chini ya uso wa nchi, wakaingia kule chini. Na yule mtu kule akiwa karibu na swichi, mara moja [Ndugu Branham anadata kidole chake—Mh.] akazima ile swichi. Na kulikuwa ni kweusi sana na ni giza, mpaka hata usingeweza kuona mkono wako ukishuka kusogea

mbele ya uso wako. Maskini msichana mdogo, kijitu kidogo, alihofu sana. Akaanza kupiga mayowe kwa nguvu zake zote, "Loo, kuna giza! Kuna giza! Kuna giza," akipiga mayowe ya kupagawa.

168 Ilikuwa kwamba kaka yake mdogo alikuwa yeye yupo amesimama. Akapiga kiyowe gizani, akasema, "Usiogope, dada yangu mdogo, yupo mtu hapa anayeweza kuiwasha taa."

169 Haleluya! Maskini Kanisa hili dogo litaenda kufanya nini? Msiwe na wasiwasi. Yupo Mtu hapa leo anayeweza kuiwasha Taa, huyo ni Bwana Yesu Kristo. Loo, naam. Bwana Yesu Kristo!

170 Kumbuka, yule kipofu. . . wa—wale matajiri katika siku za kuzaliwa Kwake Yesu, hawakutolewa nje na kupofushwa kwa mweko wa Yerusalemu walipofika huko, wakiulizia habari Zake. Thiolojia yao—thiolojia isingeweza kuelezea jambo hilo. Lakini wakati walipogeuka kando, waliifuata mpaka kwenye Nuru ya Uzima wa Milele.

171 Ninyi wafanyabiashara leo, msiangalie mieko ya madhehebu haya, bali lishikilieni Neno. Linawaongoza kwenye ile Nuru. Usiogope, dada yangu mdogo, yupo Mtu hapa Ambaye anaweza kuziwasha Taa. Yupo Kristo hapa Ambaye anaweza kulifanya Neno Lake liishi kama vile tu alivyokuwa wakati huo, kujithibitisha Mwenyewe ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

Hebu na tusimame.

172 Nina dakika kumi na tano kabla ya wakati wa kwenda kwenye ule mkutano mwingine. Je! ungetaka kuinua mikono yako na kusema, "Mungu, niwashie taa, asubuhi ya leo. Ninaamini Neno. Ninaamini mitambo. Weka Dainamikia ndani yangu, Bwana"? Inueni mikono yenu na mumlilie kwa sauti kuu, "Bwana, ziwashe Taa!" Yupo mtu hapa anayeweza kuziwasha Taa. Sisi tumekufa, katika ukomunisti, na tumeliwa na kila namna ya parare wa madhehebu, bali yupo Mtu hapa Ambaye anaweza kuziwasha Taa. Mtu huyo ni Roho Mtakatifu, Mwenyewe, Yesu Kristo aliyedhihirishwa katika Roho!

173 Bwana Yesu, gusa kila mmoja wa mikono hii; si hiyo tu, bali shuka chini mkononi ukaingie moyoni, na uiwashe Taa ya Injili. Katika Jina la Yesu!

*WASHA TAA* SWA64-0125
(Turn On The Light)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi asubuhi, tarehe 25 Januari, 1964, katika Ramada Inn kule Phoenix, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings.

SWAHILI

©2007 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org